JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKARI ZA MITAA,
HALMASHAURI YA WILAYA YA SIMANJIRO
SHULE YA SEKONDARI SIMANJIRO

S.L.P 9515

SIMANJIRO-MANYARA.

www.simanjirodc.co.tz

TAR: _____

MKUU WA SHULE: 0787030715 / 0747 22 30 66
MAKAMU MKUU WA SHULE: 0759 55 35 07

MZAZI/MLEZI WA MWANAFUNZI,
_____,
SLP_____,
_____.

MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI SIMANJIRO KIDATO CHA TANO 2022/2023.

UTANGULIZI

Nina furaha kukutaarifu kwamba mwanao amechaguliwa kujiunga na kidato cha tano katika shule hii mwaka **2022** katika **tahasusi** ya **HKL/HGL**.

Shule ya sekondari SIMANJIRO iko umbali wa **Km 188.4** kusini mashariki mwa jiji la Arusha. Usafiri wa magari kutoka Arusha mjini kuja shuleni Simanjiro unapatikana makao mapya,stendi ya mabasi ya Simanjiro kwa nauli ya shilingi **10,000/=,** magari yanaondoka **saa 4:30 asubuhi** na **saa 7:00** mchana kila siku.

Ukifika Arusha unaweza kuwasiliana kwa namba za simu zifuatazo za wakata tiketi kwa ajili ya usafiri;

- **Basi la SIMANJIRO EXPRESS- 0759734770 (mwarabu) na 0762212171 (NEEMA) saa 4:30 asubuhi**
- **Basi la ZAKARIA EXPRESS- 0767 600 026 saa 7:00 mchana.**

Muhula wa masomo utaanza tarehe -------- /…. / 2022
Siku ya mwisho kuripoti ni tarehe ---------- /…../ 2022

MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

2.1 SARE ZA SHULE

- Mashati mawili meupe yenye mikono mirefu yasioonyesha kwa ndani (non transparent) kwa WOTE-**anunue huko huko**.
- Wavulana suruali mbili (2), RANGI……**aje na Tsh 20,000/= x 2=40,000/=**
- sketi mbili (2) kwa wasichana za rangi ya …… iliyokolea,mshono wa rinda box moja kubwa nyuma na mbele (aje na hela atashonewa shuleni kwa utaratibu unaotakiwa)
- Rangi ya sweta ifanane na rangi ya suruali au sketi za shule.
- Sweta rangi ya……iwe na shingo ya V.**Aje na tsh 18,000/=** atanunua shuleni ili kuwe na rangi sawa kwa wote.
- Tai (ndefu) iwe na rangi ya suruali na sketi. (WOTE)-**aje na tsh 5,000/=** atashonewa shuleni.
- Soksi pea mbili (stocking) nyeupe kwa wasichana na **nyeusi kwa wavulana**-**anunue huko huko**.
- Viatu pea mbili rangi nyeusi vinavyopigwa rangi na kufungwa kamba visiwe na kisigino kirefu-**anunue huko huko**.
- Kwa wavulana,mkanda mweusi usio na bokoli kubwa-**anunue huko huko**.
- Kwa mabinti wa kiislamu wanatakiwa kuja na shati 02 nyeupe za mikono mirefu na hijabu nyeupe isiyo na urembo.
- T- shirt 02 za …… (shingo ya duara)-aje na **tsh 8,000/=**atanunua shuleni.

- **2.2 SARE ZA KUSHINDIA**
- Kwa wavulana Suruali mbili rangi ya ……..**(grade one)-aje na Tsh 20,000/=** @ atashonewa shuleni kwa utaratibu unaotakiwa**.**
- T-shirt 2 za rangi ya……. (WOTE) zenye kola na nembo ya shule.**Aje na Tsh 10,000/=** @ atashonewa shuleni kwa utaratibu unaotakiwa.

- **2.3 SARE ZA MICHEZO**
- Track suit pea moja (1) rangi ya KIJIVU yenye mistari myeupe pembeni na yenye nembo ya shule.(nembo itagongwa shuleni).-**anunue huko huko**
- Bukta 01 nyeusi yenye mistari myeupe pembeni na T-shirt 01 nyeusi yenye mistari myeupe pembeni kwa ajili ya michezo (isiwe na kola wala maandishi yoyote)-**anunue huko huko**
- T-Shirt Nyeupe zenye kola yenye michirizi ya blue (form six). Hizi ni kwa ajili ya kuvalia Tracksuit-**anunue huko huko**
- Kwa wasichana sketi moja fupi nyeusi yenye marinda ya kawaida kwa ajili ya kuvalia track suit wakati wa michezo.
- Raba ya michezo NYEUPE pea moja (1) na viatu vingine vya michezo-**anunue huko huko**

2.4 MAHITAJI YA BWENINI (*anunue huko huko)*

- Mashuka mawili rangi ya pinki (WOTE)
- Chandarua kwa ajili ya kuzuia mbu.
- Blanketi moja(1) kwani kuna baridi,
- Mto wa kulalia na foronya la rangi ya pink.

- Mswaki na dawa yake
- Sabuni za kufulia,

- Sahani, kikombe, Bakuli za mfupa na kijiko
- Sabuni za kuogea,
- Ndoo mbili zenye mikono.
- Jembe na mpini wake,
- Fyekeo 01
- Godoro moja futi 2.5 kwa 6
- Sanduku imara (tranka) kwa ajili ya kuhifadhi vifaa vyake bwenini,
- Fagio moja ya chelewa.
- Taulo na ndala za kuogea

2.5 ADA NA MICHANGO YA SHULE

a) **Ada ya shule** kwa mwaka ni **Tsh 70,000/=** na unaweza kulipa kiasi cha **Tsh 35,000/=** kwa muhula au ada yote kwa mara moja.Fedha hizo zilipwe kwenye akaunti ya shule ***SIMANJIRO SECONDARY SCHOOL*, NMB *ACCOUNT NUMBER 4241100003.*** (TAFADHALI ANDIKA JINA LA MWANAFUNZI KWENYE PAY IN SLIP).

b) Michango inayotakiwa kulipwa na mzazi ni:

- Shilingi **15,000/=** kwa ajili ya ukarabati wa samani.
- Shilingi **6,000/=** kwa ajili ya kitambulisho na picha.
- Shilingi **20,000/=** kwa ajili ya taaluma kwa mwaka (elfu 10 kwa mhula)
- Shilingi **30,000/=** kwa ajili ya kuwalipa wapishi, walinzi, na vibarua wengine kwa mwaka.
- Shilingi **3000/=** nembo ya shule kwenye shati la mwanafunzi.
- Shilingi **6000/=** kwa ajili ya kitambulisha cha **iCHF**,Kwa wale wenye vitambulisho vya bima ya afya waje navyo.**kama *huna bima yoyote uje na hela mkononi,usilipie benki tafadhali!***
- Shilingi **20,000/=** mitihani ya kujipima, Mock exams.
- Fedha ya tahadhari shilingi **5,000/=** *Fedha hizi hairejeshwi utakapo maliza shule.*

JUMLA ya michango yote ni Laki moja na Elfu tano tu (105,000/=).

Jumla ya michango yote pamoja na ada ni Tshs. 175,000/= kwa mwaka.

Michango hiyo pamoja na ada zote ziingizwe kwenye akaunti ya shule hapo juu isipokuwa hela ya bima ya afya **iCHF** (tsh 6,000/=)

c) Mahitaji ya lazima kwa ajili ya masomo husika.

- Vitabu vya masomo ya tahasusi husika.
- Madaftari (counter books) 10
- Kamusi kubwa ya kiingereza (dictionary).
- Begi zuri la kuwekea madaftari.
- REAM PAPER 1 (A4), isiyo na mistari kwa matumizi binafsi.

SHERIA ZA SHULE

Lengo letu ni kumjengea mwanafunzi kuwa na mwenendo mzuri na hivyo kumuwezesha kufanikisha lengo la alichokifuata hapa shuleni. Sheria hizi zitamsaidia kumletea hali ya **AMANI, UMOJA** na **FURAHA** shuleni na kumfanya kuwa raia bora.

Kila mwanafunzi aje na nia ya **KUSOMA KWA BIDII** na ajitahidi kuishi vizuri katika jumuiya ya Simanjiro Sekondari.

Vifuatavyo ni vifungu muhimu vya sheria za shule. Na kila mmoja anapaswa kuzifuata kwa ukamilifu:

- Lugha inayotumika darasani na nje ya darasa ni kiingereza tu. Hii inasaidia kuleta ufanisi katika masomo.
- Kila mwanafunzi ni lazima ahudhurie vipindi vyote vinavyompasa kama ratiba ya shule inavyoonyesha
- Kazi za mikono ni moja ya elimu inayotolewa hapa shuleni kila mmoja lazima ashiriki bila kutegea.
- Hairuhusiwi kupeleka chakula nje ya bwalo la chakula.
- Mwanafunzi haruhusiwi kuleta chakula cha aina yoyote ile arudipo shuleni toka likizo,au arejeapo baada ya kupata kibali kutoka nje, hii ni kwa ajili ya afya yake.
- **Mavazi yote ya binafsi hayahitajiki hapa shuleni,muda wote anatakiwa kuvaa sare za shule na nguo za kushindia tuu,(SHAMBA DRESS).**
- Mwanafunzi haruhusiwi kukaa na dawa yeyote ile, kwa mwanafunzi mwenye dawa atoe taarifa kwa **patron** au **matron** ili aweze kuhifadhiwa dawa zake mpaka atakapomaliza dozi atakyokua ameandikiwa na Daktari. Mwanafunzi haruhusiwi kumpa mwanafunz mwenzake dawa bwenini.
- Mwanafunzi haruhusiwi kumiliki vyombo vya muziki kama vile **radio, walkman, earphones, headphones, na vitu vingine kama vile kamera n.k**
- Wizi, matusi na ugomvi haviruhusii kabisa shuleni.
- Mwanafunzi haruhusiwi kumiliki silaha ya aina yoyote ile, kuwa na vitu vyenye ncha kali kama vile visu n.k
- Kila mmoja atawajibika kutunza kwa uangalifu wa hali ya juu vifaa vyote vya shule atakavyokabidhiwa na asivyokabidhiwa. Uharibifu au upotevu wowote utakaotokea gharama za matengenezo au fidia zitalipwa na atakayefanya uharibifu huo.
- Kila IJUMAA, JUMAMOSI, NA JUMAPILI wale waendao kusali kwenye madhehebu mbalimbali watatakiwa kuvaa sare za shule na kurudi shuleni baada ya sala zao kukamilika. Watarudi na kuendelea na ratiba za shule.

- Kila mwanafunzi anategemewa kuwa na heshima kwa watu wote hapa shuleni, kwa uongozi na wanafunzi wenzake,atumie lugha safi kwa watu wote na atatoa matatizo yake kwa viongozi wake kwa kufuata utaratibu husika.
- Ni marufuku kwenda kwenye nyumba za walimu au za wafanyakazi wa shule bila kibali.
- Hairuhusiwi kumiliki simu au kifaa chochote cha simu,laini za simu n.k.
- ***MZAZI ANARUHUSIWA KUWASILIANA NA MWANAE SIKU ZA JUMAMOSI NA JUMAPILI KWA KUPITIA NAMBA ZA SIMU ZILIZOKO IDARA YA MALEZI AMBAZO NI 0718 004880 AU 0753 06 21 75 NA SIKU YA KUTEMBELEA WANAFUNZI NI KILA JUMAPILI YA MWISHO WA MWEZI.***

MAKOSA YATAKAYO SABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE.

- Wizi.
- Kutohudhuria masomo mfululizo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa au utoro.
- Kugoma au kuhamasisha mgomo.
- Kutoa lugha chafu kwa wenzake, walimu au walezi na jamii kwa ujumla.
- Kupigana na mwanafunzi mwenzake, mwalimu,au mtu yeyote yule.
- Kufuga ndevu.
- Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya.
- Uvutaji wa sigara.
- Uasherati, uhusiano wa jinsia moja, kuoa au kuolewa.
- Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayo vunja sheria za nchi.
- Kusababisha mimba au kumpa mimba msichana.
- Kutembea katika majumba ya starehe au nyumba za kulala wageni.
- Kumiliki au kukutwa na simu ya mkononi katika mazingira ya shule,kuwa na laini ya simu n.k.
- Kudharau bendera ya Taifa na Wimbo wa Taifa.
- Kufanya jaribio lolote la kujiua au kutishia kujiua kama vile kunywa sumu n.k
- Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

N: B. Iwapo mwanafunzi atakuja na simu ya mkononi, atawajibika kuikabidhi Kwa matroni au patroni kabla hajakabidhiwa eneo la kulala, (kabla hajaingia bwenini).Atarudishiwa siku ya kufunga shule.

VIAMBATANISHO VYA FOMU MUHIMU.

- Fomu ya Uchunguzi wa Afya (medical examination form) ambayo itajazwa na Mganga mkuu wa hospitali ya serikali.
- Fomu ya maendelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi, mkataba wa kutoshiriki katika mgomo, fujo na makosa ya jinai.
- Fomu ya mzazi kukiri na kukubaliana na sheria na kanuni za shule, pia kukubali kulipa ada na michango mingine ya shule.
- Namba za simu za wazazi ama walezi.

N**: B: TAFADHARI SOMA MAELEKEZO HAYA NA MAAGIZO KWA UMAKINI ILI UWEZE KUYATEKELEZA KWA UKAMILIFU.**

GERALD DOMINICK SABUNI

Mkuu wa Shule

SHULE YA SEKONDARI SIMANJIRO

FOMU YA KUJIANDIKISHA SHULENI

TAARIFA ZA MZAZI/, MLEZI

1. **Jina kamili la baba……**
2. **Kazi yake……**
3. **Jina kamili la Mama…….**
4. **Kazi yake……..**
5. **Jina kamili la Mlezi (Iwapo mtoto haishi na wazazi wake)……**
6. **Kazi ya Mlezi……..**
7. **Nyumbani kwa Baba (alipozaliwa mtoto)**
   Kijiji/Mtaa…….. Wilaya……
   Kata…… Mkoa…….
   Tarafa……..
8. **Anwani ya Mahali pa kazi ya baba……..**
9. **Anwani ya mahali pa kazi ya mama……..**
10. **Mtoto anaishi na (i)baba tu (ii) mama tu (iii) wazazi wote (iv) walezi**
    kata isiyohusika

11. **Dini ya baba …….dhehebu……..**
    Dini ya mama…… dhehebu……
12. **Anwani kamili ya nyumba ambapo amtoto atakuwa anakwenda siku za likizo ……..**
13. **Mimi …….. Baba/mama/mlezi wa……..**
    Nathibitisha kuwa taarifa hiyo hapo juu ni sahihi na naahidi kushirikiana na walimu ili kuhakikisha kwamba kijana wangu anakua na tabia nzuri, mchapa kazi na mwenye bidii ya masoma.

Tarehe……. **……...**

Sahihi ya mzazi/ mlezi

FOMU YA KUKUBALI NAFASI NA UTII WA SHERIA ZA SHULE

Mimi …….. (jina kamili) kidato cha …… Mwaka …… nakubali/Sikubali nafasi hii/sikubali nafasi hii na ninaahidi kufuata sheria na taratibu za shule kama zilivyopangwa na endapo nitaenda kinyume na sheria na taratibu hizo nichukuliwe hatua za kinidhamu.

Tarehe……. …….
Sahihi ya Mzazi

Tarehe…….. ……
Sahihi ya Shahidi

Tarehe……. ……
Sahihi ya Mkuu wa Shule

PRESIDENT'S OFFICE,

REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT.

SIMANJIRO SECONDARY SCHOOL.

To be completed by Medical Government Hospital in a respect to all Simanjiro Secondary school new entrants 2022.

Full Name…….

Age……

i. Skin……
ii. Blood count (red and white) ……
iii. Urine Examination…….
iv. Stool examination……
v. Syphilis Test ……..
vi. T.B Test…….
vii. Ear Test……
viii. Eye Test ……..
ix. Spleen ……..
x. Abdomen ……..
xi. Additional information of any other physical mental hereditary of infection

……
……
……..

Treatment after Examination

……..

……

(Please state nature of treatment)

MEDICAL CERTIFECATE:

I certify that the above mentioned has been examined and found fit to pursue further education.

Signature……

Designation……

Station……..

Date …….. Official Stamp…….

ORODHA YA VITABU MUHIMU UNAVYOPASWA KUWA NAVYO KAMA UNAWEZA KUJINUNULIA.

A-LEVEL GENERAL STUDIES

- UNDERSTANDING ADVANCED LEVEL GENERAL STUDY
- ADVANCED LEVEL SECONDARY SCHOOL EDUCATION by Joannes and Sospeter M. Deogratias
- GENERAL STUDIES PAPER REVIEW,, any of recent years.
- RICHARD, r.f. Mbalase. General Studies for Advanced level certificate
- Mgaywa, B.M. General studies for Advanced level 3rd Ed.
- Joannes BrigiwaMungu & Sospeter. M. Deogratias. Understanding Advanced level general studies; Advanced Secondary school EEducation

A-LEVEL HISTORY I

1. Hallert, R.(1983).Africa since 1875 vol.3.East African Educational Publishers. Nairobi Kenya
2. July,R.W.(1992). A History of the African people, East Africa Education Publishers, Nairobi Kenya
3. Illife,J.(1995). Africans, the History of the continent. Edinburg, Cambridge; university press, London UK.
4. Manning, P.(1990).Slavery and African life; occidental oriental and African slave trade, Cambridge University Press.
5. Njiro, E.(1989). A History of Africa in the 19th century. Literature Bureau Nairobi, Kenya.
6. Rodney, W.(1989). How Europe underdeveloped Africa, publishing House, Dar es salaam, Tanzania
7. Shillington, K.(2004).History of Africa. Macmillan publishers. Hong, japan
8. Davidson, E. ef al (1997); The growth of the African civilization East and central Africa to the late 19th century, Longman Group Limited, Singapore
9. Freud, B.(1998): The making of contemporary Africa; The Development of African societies since 1800, Colorado, Lynne Rienner Publishers.
10. Kimambo, I and Temu, A(1969); A history of Tanzania, East Africa publishing House Nairobi, Kenya
11. Robin, H.(1993); African since 1875 1872 A modern History, East African Publishers ltd, Nairobi, Kenya
12. Roland, O. and Anthony, A.(2007).Africa since 1800, Cambridge University Press, New York, USA.
13. History for secondary schools form five (Tanzania Institute of Education)
14. History for secondary schools form six (Tanzania Institute of Education)
15. History for secondary schools: from five (TIE)
16. History for secondary schools: form six (TIE)

A-LEVEL HISTORY II

1. Nelson throne Essential modern world history
2. History of 21st century (World history)-Oxford
3. H.L. Peacock. (2010).A History of modern Europe 1789-1981. seventh Edition
4. The History of Modern World. (2007). 6th Edition. Oxford University press

A LEVEL KISWAHILI

1. VITABU VYA UCHAMBUZI

USHAIRI

- Kimbunga- H.Goro
- Fungate ya uhuru – M.S.Khatibu
- Chungu tamu – T.A. Mvungi

RIWAYA

- Vuta n`kuvute – S.A Shafi
- Usiku utakapokwisha – M.Msokile
- Mfadhili – H.Tuwa

TAMTHILIYA

- MORANI – E.Mbogo
- Nguzo mama – P.Mohamedi

2. Kiswahili sekondari – kidato cha V&VI-Oxford
3. Kiswahili sekondari – kidato cha Tano (TIE)
4. Kiswahili sekondari – kidato cha sita (TIE)

LANGUAGE I

1. Ashel, N. (2009) Advanced level English A practical Approach DSM.
2. Kadeghe, Michael (2011) The real English Textbook for Advanced level (form six) DSM
3. Kadeghe, Michael. (2011). The Real English Textbook for Advanced level: form five.DSM.
4. TIE .ENGLISH Language for secondary schools, language & usage: form five &/six papers.
5. Advanced English language: From five & six by Oxford

LANGUAGE II

1. Ashel, N. (2011).Advanced level Literature. The Essential Guide: Good Book Publishers, DSM
2. Advanced level literature. (2008).DSM. Nyambari Nyangwine publishers
3. Achebe, A.(1966) A man of the people
4. Ayi Kwei Armah .(1882).The Beautiful ones Are Not Yet Born
5. Ibsen, H.(1882),An Enemy of the people. A-DSM
6. Imbuga. F.C. (1976). Betrayal in the city
7. Mirii Ngungi & Thing`o. (1982). I will Marry When I want, DSM . EAEP
8. Institute of Education. selected poems
9. Mloka, C. (2007) .The wonderful Surgeon.
10. TIE. English language for secondary schools, literature & stylistics: form five & six .Paper 2.

GEOGRAPHY DEPARTMENT

- General Geography In Diagrams By R.B BUNNET

- Research Methodology By KOTHARI C.R
- Human And Economic Geography By MSABILA DT(For Geo.II)

- (Colin Buckle), LANDFORMS IN AFRICA
- C.R. Kothari), Research Methodology
- (H.C. Truran), A Practical Guide To Statistical Maps And Diagrams
- (Goh Cheng Leong.Gillian.C. Morgan), Human And Economic Geography

MUHIMU SANA

- ***USIJE NA NGUO ZA NYUMBANI KAMWE HAZIRUHUSIWI***

- ***UNAPOKUJA SHULE UVAE TRUCK SUIT TU NA SI VINGINEVYO.***